



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE



"TANGAZO"

SIMU NA: 026 2782111 (DED)
FAX NA: 026 2782857 (DED)
Barua pepe: ded@njombedc.go.tz

OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W),
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE,
S. L. P. 547,
NJOMBE

Tarehe: 08/11/2023

**ZABUNI YA UPANGISHAJI WA VYUMBA VYA OFISI KWENYE JENGO LILILOKUWA
LIKITUMIKA KAMA OFISI ZA TANROADS HAPO AWALI LILILOPO NJOMBE MJINI**

ZABUNI Na. LGA/031/2023-2024/HQ/NC/02

1. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe anawatangazia Wananchi wote wanaotaka/wanaohitaji vyumba kwaajili ya matumizi ya ofisi kupanga kwenye Jengo la Ofisi lililopo Njombe Mjini- Ofisi za TANROADS za zamani.

2. Maelezo ya Ofisi ni kama ifuatavyo;-

- i. Ofisi zipo kwenye majengo ya Ofisi za Ujenzi za Halmashauri ya Wilaya ya Njombe (Ofisi za TANROADS za zamani)- Njombe Mjini.
- ii. Idadi ya Vyumba ni tisa(9) na Vyoo viwili(2).
- iii. Huduma ya Umeme na Maji ipo
- iv. Aina ya Mpangaji: Taasisi binafsi (NGO's), Taasisi za Serikali, Kampuni binafsi n.k
- v. Mwombaji awe tayari kutaja gharama za upangaji wa jengo hilo kwa kila mwezi.
- vi. Ada ya maombi ya Zabuni ni Shilingi elfu Ishirini tu za kitanzania (Tsh 20,000/=).

N.B:

Jengo linapangishwa kwa matumizi ya ofisi tu, hivyo muombaji aombe kwa ajili ya matumizi hayo.

3. Waombaji wote mnakaribishwa kufika katika **ofisi ya Kitengo cha Manunuzi iliyopo Njombe mjini karibu na ofisi za TANESCO** (barabara ya Njombe – Songea) kwa ajili ya uchukuaji wa nyaraka za zabuni (Tender Document). Katika nyaraka za zabuni (Tender Document) kuna masharti na vigezo vya nyongeza za Zabuni hii.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE




4. Aidha ada itakayolipwa na muombaji ni kwa ajili ya nyaraka za zabuni (Tender Document) hii na haitarejeshwa (Non Refundable) na italipwa kwa namba ya malipo (Control Number) itakayoandaliwa na Halmashauri.

N.B: Mzabuni atatakiwa kuambatanisha/ kufika na nakala ya risiti ya ada ya maombi ili kupatiwa nyaraka za Zabuni hiyo.

5. Mwombaji awe tayari kulipia kodi ya muda wa mwaka mmoja (miezi kumi na mbili).
6. Mkataba utakuwa wa muda wa mwaka mmoja ambao utahuishwa (Re-newable) pindi unapoisha muda wake.
7. Maombi yote yakiwa na nyaraka tatu, nyaraka moja katika uhalisia wake (Original) na zingine mbili zikiwa vivuli (copy) yafungwe kwa lakiri na kuandikwa namba ya zabuni juu ya bahasha na kuwasilisha katika Ofisi ya Kitengo cha Manunuzi Halmashauri ya Wilaya ya Njombe iliyopo Njombe mjini karibu na TANESCO (barabara ya Njombe – Songea) kwa njia ya mkono.

Juu ya bahasha iandikwe anuani ifuatayo;- **KATIBU BODI YA ZABUNI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE,
S.L.P 547,
NJOMBE.**

8. Mwisho wa kurudisha kotesheni ni tarehe **15/11/2023** siku ya **Jumatano saa 4:30 Asubuhi.**
9. Ufunguzi utafanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe (Njombe mjini karibu na TANESCO) siku ya **Jumatano tarehe 15/11/2023** kuanzia saa **5:00 Asubuhi.** Waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa kushuhudia ufunguzi utakaofanyika siku hiyo.
10. Waombaji wanatakiwa kufika Ofisi ya Kitengo cha Manunuzi Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kwa ajili ya kuchukua nyaraka za zabuni (Tender Document) kuanzia Jumatano tarehe **08/11/2023** na kurudisha kabla ya muda wa mwisho kumalizika (**saa 4:30 Asubuhi**) siku ya **Jumatano tarehe 15/11/2023.**


Christopher A. Sanga
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA NJOMBE

**MKURUGENZI
HALMASHAURI YA WILAYA
NJOMBE.**